Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

JUZU 82 No. 237 | RAJAB - SHABAN. 1444 AH | FEBRUARI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Watu Wenye Ubora – Hadhrat Hamzah[ra] na Maombi Kwa Mwaka Mpya

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu

Baada Ya Kusoma *Tashahhud, Tawwudh* na *Surah Al Fatiha* Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba baada ya kukamilisha maelezo ya maisha ya Hadhrat Abu Bakr (ra), alisema kwamba kulikuwa na baadhi ya Masahaba ambao maelezo zaidi yangeongezwa kuhusiana nao katika uchapishaji wa hotuba hizi. Hata hivyo, Hudhur (atba) alisema kwamba watu wengi wamekuwa wakimwandikia, wakimweleza ni kiasi gani wamefaidika kwa kusikiliza hotuba hizi. Kwa hiyo, Hudhur (atba) alisema kwamba aliona ni vyema kutaja maelezo haya zaidi katika hotuba zake vile vile, ili kwamba idadi ya juu zaidi ya watu iweze kufaidika nazo.

Mapenzi ya Mtume Mtukufu (s.a.w) kwa Jina la Hadhrat Hamzah[ra]:



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tanoatba akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 30 Disemba, 2022. Akieleza Watu Wenye Ubora – Hadhrat Hamzah (r.a) na Maombi Kwa Mwaka Mpya

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kwanza atamtaja Hadhrat Hamzah (ra). Alikuwa ni ami wa Mtume Mtukufu (s.a.w) na alipendwa sana naye. Imesimuliwa kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) alipenda jina la Hamzah. Wakati fulani, mtu mmoja alimwuliza Mtume Mtukufu (s.a.w) wampe jina gani mtoto wao mchanga; Mtume Mtukufu (s.a.w) alimshauri kumpa mtoto huyo wa kiume jina la Hamzah bin Abi Muttalib kwani alilipenda jina hilo. Hudhur (atba) alisema kwamba Hadhrat Hamzah (ra) pia alijulikana kwa jina la Abu Ammarah, baada ya kuzaliwa kwa binti yake Ammarah kutoka kwa mke wake wa pili Khaulah. Hadhrat Hamzah (ra) pia alikuwa na binti mwingine aliyeitwa Umamah. Imeandikwa kwamba kwa kuzingatia Mkataba wa Hudaibiyah, ulipofika wakati wa Mtume Mtukufu (s.a.w) kuondoka Makka, Umamah alikuja akikimbia nyuma ya Mtume Mtukufu (s.a.w). Hadhrat Ali (ra) alimchukua na kumkabidhi Hadhrat Fatimah (ra) na akamtaka amtunze. Baada ya hapo, Hadhrat Ali (ra), Hadhrat Ja'far (ra) na Hadhrat Zaid (ra) wote walitaka kumweka chini ya uangalizi wao. Suala hilo lilipelekwa kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) aliyesema kwamba yafaa abaki chini ya uangalizi wa mama yake mdogo, kwani mama mdogo ni kama mama. Hudhur (atba)

Endelea Uk wa 3..

Maono ya Huzur yatimia: tunayo, Amri Abedi Studios - Dar es Salaam, Tanzania

Na. Sheikh Shaban A. Shunda

"Uwepo wa studio za MTA International Tanzania Amri Abedi studio ni maono ya Hadhrat Khalifat ul Masihi wa tano (atba)" ni maneno yaliyotamkwa na mratibu mkuu wa studio hizo Maulana Asif Mahmood Butt katika ufunguzi rasmi wa studio uliofanyika jijini Dar es salaam katika ukumbi wa msikiti Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania uitwao Masjid Salaam mnamo tarehe 24/12/2022.

Ufunguzi huu umetokea baada ya upevukaji wa maono haya yaliyochukuwa miaka mitano mpaka kufikia hapo, Hapa tunajifunza kitu kikubwa sana, katika mafanikio ya jambo lolote, wengi hupewa au hupata mawazo mengi chanya ya mafanikio, ila wanashindwa pindi wanaposubiria wakati sahihi na mahali sahihi pa kuyafanyia likue basi inachotakiwa kufanya ni ulipatapo tu uanze kulifanyia kazi na kulibadilisha kuwa zao, utakapoanza kujishauri basi milango mingi ya haiwezekani huendelea kufunguka.



Picha ya pamoja siku ya ufunguzi wa MTA Studios Dar es Salaam, kulia akiwa ni Katibu Mkuu Seif H. Nakuchima, wa pili Maulv Faiz Ahmad Nasir Sahib, wa tatu Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib na nne Naib Amir Maulana Sheikh Abdul-Rahman M. Ame Sahib.

Katika mlolongo huu markazi iliendelea kutuma wataalamu kuja kuandaa watu ambao wa majukumu katika vipimo vyake, kwa kumbukumbu tu alishawahi kuja bwana Umari Safiri (Mananger director of MTA Africa), Bwana Taukeel Mirza ambaye alikuja kutoa mafunzo kwa timu ya kwanza kabisa iliyoandaliwa kwa ajili ya MTA Tanzania, na alikuja na vifaa pia kwa ajili ya kurekodia, ambapo baada ya ujio wake vipindi kadhaa na mashairi yalirekodiwa katika sehemu ya chini ya jengo la zamani la makazi ya wabashiri na ofisi za makao makuu, na pia huko Morogoro ofisi ya Dawati la Kiswahili ilitumika katika kazi hii, lakini mara nyingi kwa sababu za hapa na pale za ubora waliotakiwa, vipindi hivyo vilikuwa havichezwi MTA International.

Tunakumbuka kuwa mwaka 2016 Hadhrat Amiir ul Muuminiin alifungua rasmi idhaa ya MTA Africa maalumu kabisa kwa ajili ya kuwahudumia Waafirika, idhaa hii iliongeza mkandamizo wa majukumu katika mabega ya

Endelea Uk wa 4..

Hutuba ya Huzur ya kwanza 2023 uk. 3...

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Pembe zote za Dunia

Taratibu kwa kutumia jicho la akili, tua katika sehemu iliyopembezoni kabisa mwa nchi hiyo inayoitwa India. Pembezoni hapo kuna Kijiji kiitwacho Qadian. Kama vilivyokuwa vijiji vyote chini ya Ukoloni, hakina barabara njia ya reli haipiti huko, inakubidi kutembea Maili kadhaa ili kupata Posta ilipo. Hakuna kituo cha Polisi. Ni Kijiji ambacho kimeungana na sehemu nyingine za India kwa jina tu. Hatuwezi kukosea tukisema kuwa hiki ni kisiwa.

Katika Kijiji hiki kidogo inainuka sauti na kusema kuwa ametumwa na Allah kurejesha Islam kama ilivyokuwa wakati wa enzi za Mtukufu Mtume Muhammadsaw kujenga mawasiliano baina ya Muumba na viumbe wake na kuwakumbusha binadamu wajibu wao kwa muumba wao. Na wajibu kwa viumbe wa Allah[sw]. Sauti hii inapingwakwanguvuzote.Inatangazwakwamba kwa kutangaza kuwa yeye ni Mtume ametoka katika Islam. Wimbi la upinzani linapata nguvu na kuongezeka. Mishale ya kila aina inatupwa kwa huyu Simba wa Allah lakini kama ilivyo desturi haiwi haitakuwa Simba kumkimbia Fisi. Anaendelea kutangaza kwa nguvu zaidi.

Zikiwa bado hasira zimepanda anaweka msumari wa moto kwenye donda. Anaeleza wapinzani wake na Binadamu kwa ujumla kwamba amepata Wahyi kutoka kwa Allah[sw] – Unaosema kwamba "nitafikisha ujumbe wako pembe zote za Dunia" Hili linawaongezea wapinzani kiburi na kebehi. Ndio kwanza wanaongeza kucheka na kumfanyia Shere.

Lakini kama ilivyo desturi ya Allah[sw] kinachoonekana hakiwezekani kinawezekana. Njiwa anataga Yai juu ya mlango wa Pango na maadui hawaamini kuwa mtu anayeweza kupita na kuingia ndani. Watu dhaifu, wasio na uzoefu na vita wakiwa na Silaha duni wanawachachafya makureishi walio wengi na Silaha bora kabisa. Muujiza kama huo amepewa Masih aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as], kwa kupitia muujiza MuslimTelevision Ahmadiyya, ujumbe wake umeenea Duniani kote.

Ufunguzi wa Amri Abedi Studios, Dar es Salaam kituo kitakacho tumikia Afrika Mashariki ni dalili nyingine ya kutimia kwa bishara aliyopewa Masih aliyeahidiwaas. Kupatikana kwa neema kuna kuja na wajibu. Tunatakiwa sasa tujenge utamaduni wa kuhakikisha kuwa tuna MTA majumbani mwetu na inatumika katika kutuelimisha. Tunao wajibu wa kutoa maoni ili kuboresha vipindi vinavyotolewa. Wasomi na wataalamu wetu wanawajibu wa kutumia neema waliyopewa ili wanufaike watu wengi Zaidi.



QUR'AN TUKUFU

اِنَّمَا يَعْمُرُ مَسٰجِدَ اللّٰهِ مَنْ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَاَقَامَ الصَّلٰوةَ وَ اٰتَى الزَّكٰوةَ وَلَمْ يَخْشَ اِلَّا اللّٰهَ فَعَسٰٓى اُولٰٓئِكَ اَنْ يَّكُوْنُوْا مِنَ الْمُهْتَدِيْنَ

Tafsiri:
Anayestawisha misikiti ya Allah ni yeye tu amuaminiye Allah na Siku ya mwisho, na kusimamisha Sala na kutoa Zak ana hamuogopi yeyote ila Allah; basi hao huenda wakawa miongoni mwa walioongozwa. (Sura At-Toba 9: 18)

NUKUU YA HADITHI

Hadithi:
Imesimuliwa na Hadhrat Uthman bin Affan (r.a) ya kwamba yeye aliwahi kumsikia Mjumbe wa Allah (saw) akisema: Yule anayejenga msikiti kwa ajili ya Mungu, Mwenyezi Mungu Atamjengea (nyumba) mfano wake katika Pepo. (Muslim)

Mwana Aliye Aliyehaidiwa Na Mapinduzi Nchini

Na Mwandishi Wetu

Hakuna mwenye ubavu wakubisha kuwa Mwana aliyeahidiwa Hazrat Bashir-ud-Din[ra] hali ya Islam nchini ilikuwa mbaya kuliko maelezo. Na kama angekuwa binadamu basi mahali pake pangelikuwa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi.

Islam ilikuwa imechafuliwa kiasi hiki ya kwamba hapakuwepo tofauti yoyote baina ya Mila na hicho walichokuta Islam. Hirizi zilivaliwa mwili mzima nakuwekwa mlangoni kwa ajili ya ulinzi. Wake za watu walikogeshwa maji mara wanapotoka kwenye hedhi. Mtu alikunja uso na kukasirika ulipokosa kumwamkia Shikamoo, Hotuba za Ijumaa zilitolewa katika lugha ya Kiarabu na hivyo kuwafanya wengi wabaki kukoroma na kutokokwa udenda wakati wa sala. Akina mama walipigwa marufuku kwenda Msikitini walitakiwa waswalie ndani. Kurani Tukufu ilisomwa kwa kughani bila kujisumbua kuelewa maana za ndani za Sharia hiyo ya mwisho kwa binadamu. Maulidi ilijikita katika kueleza mambo ya kimwili bila ya kugusa mambo ya kiroho ambayo ndipo shabaha kubwa ya kuja kwa Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Mwezi wa Ramadhani watu walinuka midomo kwa kutopiga miswaki eti wamefunga, Usiseme kuhusu kutema mate yalitapakaa kwani haikuruhusiwa kamwe kumeza mate. Daku ilikuwa ni saa tatu na wakati mwingine wote walikuwa wakicheza Karata tu, hakutakiwa kufikiria na kudadisi jibu la tatizo lolote ni kwamba "amesema Sheikh". Na ni hao Masheikh waliopokea kwa mikono miwili Tafsiri ya Padre Dale iliyokashifu Mtume Muhammad[saw] na Islam kwa ujumla. Hii ndio ilikuwa hali ya Islam kabla ya 1934.

Kufika kwa Askari wa Masihi Aliyeahidiwa aliyemtuma Khalifatul Masihi wa (II)[ra] **Hazrat Al-Hajj Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra]** kulileta mabadiliko na mapinduzi makubwa nchini. Tatizo letu binadamu ni kwamba tuna sahau upesi, hivyo ni muhimu sana kukumbushana kwani kukumbusha kunafaa. Islam safi isiyo na doa ilienezwa na Sheikh Mubarak Ahmad. Islam safi imeelezwa katika Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiswahili iliyo tolewa Mwaka 1953.

Sheikh Mubarak aliendelea kuongozwa na Mwana Aliyeahidiwa katika kila hatua ya yale aliyo yafanya nchini. Mara kwa mara Sheikh Mubarak alimuomba Mwongozo na maombi ya Mwana aliyeahidiwa ndiyo yaliyo leta mabadiliko makubwa nchini mwetu, Hoja ya kuheshimu Dini za watu wengine. Amani na Mapenzi ya Mungu kwa watu. Yote hayo yalisaidia kujenga utamaduni mpya ambao umeifanya Tanzania kuwa nchi ya Kupigia mfano. Watu wanao fanya utafiti wakina kuhusu siasa na utamaduni wa nchi hii wanakubali athari kubwa ya Sheikh Mubarak kwa viongozi wa baadae wa nchii hii ambao aliwafundisha Shule ya wavulana Tabora.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Watu Wenye Ubora – Hadhrat Hamzah[ra] na Maombi Kwa Mwaka Mpya

Kutoka Uk wa 1..

alisema kwamba hata mambo madogo kabisa yamefafanuliwa, kama hili linalojibu swala hili kwamba kwa nini watoto hupewa dada za mama zao au nyanya zao wakati mambo fulani muhimu yanapopelekwa kwa kadhi. Hudhur (atba) alisema kwamba mwanzoni, Hadhrat Hamzah (ra) alijiunga na Uislamu kwa mkono wa Mtume Mtukufu (s.a.w) kwa hasira na baadaye alijuta kwa kuacha imani ya mababu zake. Hakuweza kulala usiku huo, na hivyo akaenda kwenye Ka'aba na akaomba ili mashaka yake yaondolewe. Alikuwa bado hajamaliza kusali, kwamba moyo wake ulitulia na alishawishika, ambapo alikwenda kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) na kumsimulia tukio zima. Alipolisikia, Mtume Mtukufu (s.a.w) alimwomba Mwenyezi Mungu Amjaalie Hadhrat Hamzah (ra) uthabiti.

Mshika Bendera katika Misafara Mbalimbali:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba katika Safar 2 AH, Mtume Mtukufu (s.a.w) alimpatia Hadhrat Hamzah (ra) bendera ya Kiislamu katika msafara wa kuelekea Banu Zamrah huko Ghaddan. Mtume Mtukufu (s.a.w) alizungumza na chifu wa kabila hilo lililoleta mapatano ya amani kati yao na Waislamu. Hapa pia palikuwa mahali pale pale alipokuwa amefariki mama wa Mtume Mtukufu (s.a.w).

Hudhur (atba) alisema kwamba katika Jamadi al-Ula 2 AH, Mtume Mtukufu (s.a.w) aliondoka na kundi la Masahaba 150-200 Muhajiriin kuelekea Ushairah na katika safari hii, alikuwa Hadhrat Hamzah (ra) tena aliyekuwa amebeba bendera nyeupe ya Mtume Mtukufu (s.a.w). Msafara huu pia ulipelekea kuanzishwa kwa mkataba wa amani. Hudhur (atba) alisema kwamba mwanzoni mwa Vita vya Badr, Maquraish waliitisha vita vya mwanajeshi mmoja mmoja, ambapo Mtume Mtukufu (s.a.w) alimtuma Hadhrat Hamzah (ra), Hadhrat Ali (ra) na Hadhrat Ubaidah (ra). Wote wawili Hadhrat Hamzah (ra) na Hadhrat Ali (ra) walishinda kwa urahisi katika vita vyao lakini Hadhrat Ubaidah (ra) alijeruhiwa vibaya sana na alikufa kishahidi kutokana na majeraha yake alipokuwa akirejea kutoka Badr. Hudhur (atba) alisema kwamba wakati fulani, kabla ya kuharamishwa kwa pombe katika Uislamu, Hadhrat Hamzah (ra) alilewa na ilikuwa katika hali hii ambapo aliwaua ngamia wawili wa Hadhrat Ali (ra). Mtume Mtukufu (s.a.w) alifahamishwa juu ya hili na hivyo akaenda kwa Hadhrat Hamzah (ra) na kueleza kukerwa kwake. Hadhrat Hamzah (ra) alikuwa bado amelewa na hivyo akasema kwamba kila mtu alikuwa mtiifu kwa mababu zake. Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba ilikuwa bora kutozungumza naye akiwa katika hali hii. Baadaye, pale pombe ilipopigwa marufuku katika Uislamu, Hadhrat Hamzah (ra) aliiacha mara moja. Hudhur (atba) alisema kwamba hii inaweka mfano mzuri kwetu. Wakati fulani kunapokuwa na maagizo, baadhi ya watu husema kwamba wanahitaji muda wa kuitikia amri hiyo, hata hivyo mara tu amri hii ya kuharamishwa iliposikika, Masahaba hawakupoteza muda na hawakuuliza maswali kabla ya kuitikia kwa moyo wote. Hudhur (atba) alisema kwamba Hadhrat Hamzah (ra) pia alikuwa mshika bendera wakati wa msafara wa kuelekea Banu Qainuqā, ambao tayari walikuwa wanapanga mauaji ya Mtume Mtukufu (s.a.w). Baada ya Vita vya Badr, Banu Qainuqā walikuwa wa kwanza miongoni mwa Mayahudi huko Madina kuvunja mapatano yao na Mtume Mtukufu (s.a.w) na wakaanza kuleta matatizo na kupanga njama dhidi ya Waislamu. Licha ya matamshi ya chuki ya Mayahudi, Mtume Mtukufu (s.a.w) aliendelea kuwa na subira. Kwa kweli aliendelea kuwaheshimu Mayahudi. Wakati fulani, mwanamume mmoja Myahudi alimtanguliza Hadhrat Musa (as) juu ya mitume wote, na Sahaba mmoja alimjibu kwa ukali. Wakati suala hilo lilipopelekwa kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema wasimpe ubora yeye Mtume (s.a.w.) juu ya Hadhrat Musa (as) mbele ya Mayahudi, iliyokuwa ishara nzuri ya kujali hisia za Myahudi huyo. Kulikuwa na tukio lingine ambapo mwanamke wa Kiislamu alikwenda kwenye duka la mfanyabiashara wa Kiyahudi, aliyemfanyia mambo yasiyofaa mwanamke huyo wa Kiislamu hata kuweka mwiba kwenye nguo zake bila huyo mwanamke kujua ili akiondoka basi nguo zake zivuke. Waislamu walipowaendea Banu Qainuqā ili waache tabia hiyo, walijibu kwa hasira, wakiwaambia Waislamu kwamba wasiwe na kiburi juu ya ushindi wao katika Badr, kwani wasingepata matokeo haya kama wangepigana nao. Hudhur (atba) alisema kwamba hatimaye, Mtume Mtukufu (s.a.w) aliizingira ngome ya Banu Qainuqā na wakati hawakubaki na njia yoyote, ilibidi wasalimu amri. Ingawa, kwa mujibu wa sheria zao wenyewe za Musa (as) wote wangepewa adhabu ya kifo kwa ajili ya hiana yao. Lakini Mtume Mtukufu (s.a.w) akawa na huruma kwao na akawaambia wahamie mahali pengine. Kwa hiyo, Hadhrat Ubadah bin Samit (ra) alikabidhiwa jukumu la kuwatafutia Banu Qainuqā makazi mapya. Hudhur (atba) alisema kwamba baadhi wanadai kwamba wakati Banu Qainuqā walipofungua milango ya ngome yao, Mtume Mtukufu (s.a.w) alikusudia kuwaua wanajeshi wao, hata hivyo jambo hilo haliwezi kuwa kweli hata kidogo, kwani walifungua tu milango yao baada ya kuhakikishiwa kwamba maisha yao na ya wake zao na watoto wao yataokolewa. Ingawa walikuwa wanastahiki adhabu ya kifo, Mtume Mtukufu (s.a.w) aliwatendea kwa huruma na hakuwaadhibu hivyo. Kwa hivyo, madai haya ni ya uwongo kabisa.

Mauaji ya Kishahidi ya Hadhrat Hamzah (ra):

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Hamzah (ra) aliuawa kishahidi katika Vita vya Uhud, jambo ambalo Mtume Mtukufu (s.a.w) alikuwa amebashiriwa. Wakati fulani, Mtume Mtukufu (s.a.w) aliota ndoto alimoona ncha ya upanga wake ikivunjika, na aliifasiri kuwa ina maana kwamba mtu mashuhuri wa familia yake atauawa kishahidi. Mwili wa Hadhrat Hamzah (ra) ulikatwakatwa kikatili, jambo ambalo lilimsababishia Mtume Mtukufu (s.a.w) maumivu makali sana. Imesimuliwa kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) aliumizwa sana na mandhari hayo, hata akala kiapo kuwa kama angeweza, angefanya vivyo hivyo kwa watu thelathini kutoka kwa Maquraishi. Ilikuwa ni juu ya hili kwamba Aya ifuatayo ya Kurani Tukufu iliteremshwa: **"Na mkijilipiza, basi jilipizeni sawa na vile mlivyoonewa; na kama mkisubiri, hakika huo ni ubora kwa wanaosubiri."** *(Surah An-Nahl 16:127)*

Hapo Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba ataendelea kuwa na subira na akatoa kafara kwa yale aliyoyasema. Hudhur (atba) alisema kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) na familia yake walionyesha uvumilivu wa kipekee juu ya kifo cha kishahidi cha Hadhrat Hamzah (ra). Kando na kutokwa na machozi yaliyokuwa ya asili, hakukuwa na kilio au majonzi kupita kiasi. Hapo awali, Mtume Mtukufu (s.a.w) hakumruhusu Hadhrat Safiyya (ra) kuuona mwili wa Hadhrat Hamzah (ra), hata hivyo kwa nadhiri yake ya subira aliruhusu na alibakia mkweli kwenye ahadi yake. Mtukufu Khalifa (atba) alisema kwamba nyongeza hii inamalizia maelezo ya Hadhrat Hamzah (ra) na ataendelea kuwataja Masahaba wengine katika siku zijazo.

Maombi kwa ajili ya Mwaka Mpya:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kuwa mwaka mpya unaanza katika siku mbili zijazo. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Ajaalie baraka zake kwa ujio wa mwaka huu mpya. Mwaka huu mpya uwe wa baraka kwa Jumuiya. Njama na hila zote za maadui zikatishwe. Waahmadiyya kote ulimwenguni watimize madhumuni ya maisha yao kuliko wakati mwingine wowote. Hudhur (atba) pia alihimiza kufanya maombi kwa ajili ya dunia nzima; Mwenyezi Mungu Ainusuru dunia na vita. Hali za dunia zinaendelea kuzorota na dunia imesimama kwenye kilele cha maangamizo. Kila mtu anaonekana kutotamani chochote ila faida yake binafsi; Mwenyezi Mungu Awarehemu. Hudhur (atba) pia aliamrisha kuwaombea wale Waahmadiyya wote wanaovumilia dhuluma na mateso; Mwenyezi Mungu Awalinde Wanajumuiya wote dhidi ya dhuluma na ukatili katika mwaka mpya.

Endelea Uk wa 4..

Amri Abedi Studios - Dar es Salaam, Tanzania

Kutoka uk. 01

Waahmadiyya Afrika, kipindi hiko nilikuwa Jamia na niliona wanafunzi wenzangu walipokuwa hawalali wakijiandaa na vipindi vya MTA kwani makao makuu madogo ya Idhaa hii yapo nchini Ghana. Binafsi nilipata bahati ya kurekodi matangazo mawili tu ambayo mpaka sasa yanatumika, na sikuwa mshiriki wa heka heka zile za usiku na mchana walizokuwa wamebarikiwa mwenzangu. Hivyo basi Waswahili pia walitakiwa watanue mbawa zao na kufikiria kupaa zaidi kwani MTA ilikuwa changa na haina maudhui mengi hasa ya Kiswahili kwa ajili ya watu wanaongoa lugha hio. Kama nilivyoainisha kuwa ujenzi ulifanyika huko Morogoro na Wataalamu walitumwa kwa ajili ya kuwafunza watumishi, mwanzoni alitumwa bwana Zakki Sahib alikuja na vifaa na kuvifunga na kutoa mafunzo kwa ajili ya kuanza kurekodi, baada ya hapo alitumwa bwana Masoud ambaye alikuwa ***Graphic Designer*** na kuja kuipika timu katika uwanja huu.

Katika uchaguzi wa watu watakaotumikia MTA, mchakato wake sikujua ulinifika aje' lakini nilipomaliza masomo Jamia Int. Ghana 2017 na kuanza safari ya kurudi nyumbani nilipo Ossu Accra makao makuu ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Ghana, nilikuwa na mipango yangu mkakati ya kuwa sheikh katika kona Fulani niliyokuwa naiwaza huku kichwani nikiwa na mipango ya ndoa ya haraka, hapo ndipo nilipoanza kusikia fununu kuwa ninaenda Tanzania na kurudi tena nchini Ghana, kuna kijana alinifuata na kuniambia nimesikia unaenda na utarudi Je umepata taarifa hii, nakamjibu "Ndio! nimeipata kwako Ahsante". Kiukweli sikutaka kuuliza na wala hakuna aliyekuja kuniambia kuwa ipo hivi na hivi, lakini nilipofika Tanzania nikaambiwa Mjomba umefika! una wiki mbili za kusalimia na kurudi Ghana katika Studio za MTA kwa ajili ya mafunzo, basi ndipo nilirudi tena kuiandika hio historia kwani Mimi na Bwana Nurdeen Okubena wa Nigeria ndio tulikuwa watu wa kwanza kupata mafunzo katika studio zile na kwenda kutumikia nchi zetu katika uwanja huu baada ya mafunzo ya miezi mitatu na uzoefu usiofutika moyoni mwangu.

Nilipofika niliambiwa kuwa Osama Hanif Mpogo naye ni miongoni mwa watu watakaotumikia, kuwaibia siri ni kwamba bwana huyu alisubirishwa kwa takriban miaka miwili ambapo hakuweza tena kufanya chochote katika mipango yake ya utafutaji, na kipindi hiko alikuwa akitumika na uongozi wa Amiir na Mbashiri katika shughuli kadhaa za kinchi na katika matukio ya kitaifa pia. Hivyo basi alikuwa akinitembelea Morogoro wakati tukijipanga kuanza shughuli za kistudio rasmi, na katika mwanzo mwanzo huo alitumwa Bwana Ghalibu Amiri Kaluta (Presenter Ghalib) ambaye tukawa naye kwa muda fulani mpaka alipohitajika kwa ajili ya Redio Ahmadiyya Mtwara. Kazi ya kurekodi na kuratibu vipindi ni shughuli inayohitaji watu na wasaa mpana hivyo ilibidi watumishi waongezeke, hapo ndipo alipopatikana Bwana Muhammedi Higiro ambaye alipendekezwa na Bwana Osama Mpogo. Kipindi taarifa zinamfikia alikuwa anafanya kazi Kariakoo na alikuwa anatengeza hela nzuri inayomtosha na kukidhi mahitaji yake, alikuwa anafanyakazi katika kiwanda binafsi cha uchapishaji na harakati za kuweka chapa katika nguo, kwa njia ya kuchora na pia kuandika maandishi kazi ambayo walikuwa wakishirikiana na rafiki yake huko Kigamboni. Basi alipoitwa na kupewa uchaguzi kuwa afanye kazi kwa muda au kujitolea maisha Waqfu aliamua kujitoa waqfu kabisa bila kusita. Nataka niwaibie siri hapa, alipokuwa anafanya kazi ya uchapishaji na rafiki yake walifikia maazimio ya kufungua kampuni kwa pamoja na walishafanya mchakato wa mwanzo wa usajili, hivyo kuondoka kwake kulifanya jambo lile kukwama na kupata hasara ya fedha za usajili na michakato mingine, kitu kilichomfanya awe yupo kwenye deni la kumrudishia mwenziwe fedha zake au nusu hasara ya mwenzie aliyotoa katika mchakato ule. Hivyo katika kila mwezi alitoa kiasi Fulani katika posho aliyopata ili kujikomboa kwenye deni lile kwa sababu ya kuua wazo la kampuni, kana kwamba alikuwa anajinasua duniani ili kujitoa Waqfu.

Katika harakati za ujenzi na uwekwaji wa vifaa vya studio mjini Morogoro, walimu wa matawini walikuwa wanakuja kutembelea na kuangalia wakati walipokuwa wanakuja kwa ajili ya vikao vya mwezi, Mwalimu Masihi Muhammad Mrope aliambiwa abaki kwa muda na akajikuta anasaidia kazi za ujenzi wa studio, taarifa rasmi aliyopewa ni kwenda kufuata familia yake na kuhamia rasmi Mjini Morogoro tena alipewa siku zinazohesabika tu, bila shaka kuna alivyopoteza lakini vyote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Wote tulimkuta Sheikh Asif Mahmood Butt akiwa Sheikh wa Mkoa na pia Mratibu wa studio za MTA, katika maongezi Fulani alisema kwamba "Kiukweli huwezi kujua Mungu amekuandalia nini katika maisha" kwani maulana alipokuwa mwanafunzi katika Jamia Ahmadiyya Pakistan alishatumikia sana MTA na pia alishaenda kwa ajili ya mafunzo maalum huko nchini London akiwa na Maulana Sheikh Farid Tabbasam aliyemalizia utumishi wake Mkoa wa Tanga, lakini kwa kuwa Tanzania hakukuwa na Studio basi walifanya mafunzo na kuja kuendelea na masuala ya Mahubiri na malezi.

Hivyo ofisi ikafanya kazi sawa ikiwa na idara zote kwa usimamizi wa mtu mmoja moja, Sheikh Asif Mahmood Butt (Mratibu Mkuu) Mwalimu Masihi Muhammad Mrope (Meneja wa Ofisi) Sheikh Shabani A Shunda (Muandaaji wa Vipindi) Bwana Osama Mpogo (Msimamizi wa Uzalishaji) Bwana Muhammed Higiro (Mhariri Mkuu) na chini ya hawa wapo wengi wanaojitolea na kujifunza katika studio hizi.

Studio ilipokuwa mjini Morogoro tulifanikiwa kurekodi vipindi vingi vya aina mbali mbali ambavyo vinaendelea kuonyeshwa katika MTA Africa na watu walikuwa wanajitolea haswa katika jambo hili, nakumbuka siku moja ilikuwa tumepewa lengo la kurekodi vipindi maalum kwa ajili ya mwezi wa ramadhani, kiuhalisia huwa ni vipindi vinne, kilichotokea lengo lilichelewa kutufikia hivyo tukajikuta tunasiku nne mkononi mpaka vipindi vifike London, hapo kuna kuandaa kipindi, kuandaa washiriki na mazingira ya Studio, kurekodi na kuedit hivyo vipindi, kisha kuvipitia na kuvisahihisha tena upya na kujiridhisha tena na kuviwasilisha London, ukiangalia kwa umakini kwa kujua mazingira halisi hili ni jambo la kuchekesha kama kudhani linaweza kufanyika ndani ya siku nne, hivyo basi kazi ilianza rasmi na maandalizi ya mwanzo yalichukua siku moja na nusu na Mada ziliwafikia Mwalimu Rundo na Mwalimu Shamuni Mwishehe Juma muda wa Mchana na simu za kuwataka waje usiku baada ya kumaliza kufanya vipindi vya Jamia ili kurekodi vipindi viwili, kilichofuata mbele ilikuwa ni wakati wa mvua na mvua ilinyesha vilivyo, tulifunga studio saa kumi alasiri na kwenda kupumzika kidogo na kurudi wakati wa magharibi, tuliporudi studio mvua kali zaidi ikanyesha, Walimu wakaamini kipindi kitaakhirishwa na hata baadhi ya sisi tukajua kifuatacho ni kwenda kulala, lakini kwa umuhimu wa kuwasilisha vipindi maalum sawa na wakati mawazo hayo yalikuwa sio sahihi. Niliwapigia walimu na kuwaambia wawe tayari lakini hawakuchukulia kwa uzito, na watu wa studio tukaanza kurudishiana maneno ya kwanini hivi kwanini vile ila ilikuwa ni ya kujenga, mwisho Maulana Asif Sahib aliwasha gari na kuwafuata na mvua ile, Mwalimu Rundo walimkuta kavalia msuli anakula ugali wake bila wasi wasi na Maulana Shamuni Sahib alishaanza harakati za kulala, maneno yaliongolewa huko nilistahiwa yasinifikie kwa sababu ni Sheikh tu lakini nilionekana nimechangayikiwa na walikuja kwa sababu ni kazi ya Mungu tu. Kwa fadhila za Mungu tulifanya kazi kwa tabasamu zote na tukamaliza saa tano na nusu usiku na tukaenda kula chakula kwa pamoja na kila mtu akarejea nyumbani kwake. Nyakati ngumu zilikuwepo nyingi na furaha ilikuwa humo humo kwani kila aliyefanya kazi alifanya kwa furaha na ili kupata radhi ya Allah. Kitu kikubwa na kigumu ilikuwa kuunda watu ambao wangeweza kuongea katika vipindi na kusaidia wakati wa uzalishaji, katika mafunzo wengi huwafundisha watu kana kwamba wanajua kama yeye afundishe, hivyo kuanza kuleta maneno ya huyu haelewi, huyu hafai na kadha wa kadha. Hivyo basi ugumu nilioufanya Mimi katika kuwafundisha watu niliokuwa ninaowahitaji ni kuwafundisha katika wakati wangu wa faragha na kujenga nao urafiki, jambo kubwa tulilofanikiwa ni kuwaandaa wanafunzi wa Jamia kuendesha kipindi chao maalumu kuhusu maisha ya Mtume (sa) na naweza sema wanafunzi wale walioshiriki na kupita MTA wana maendeleo mazuri huko wanakotumikia kwani walifadika kujifunza nje ya darasa kuliko wenzao.

Vipindi vya wakina mama vilihitaji uangalizi maalumu kwa sababu ya majukumu yao na silka zao, kwa mfano tuliandaa kipindi Kiitwacho **Islam mkombozi Wangu** maandalizi ya mwenzo tuliawa andaa washiriki vyema na tukamaliza lakini ilipofika wakati wa kurekodi asilimia sitini ya washiriki wote walikuwa wana udhuru hivyo ilibidi kuwaandaa wengine kwa ajili ya kurekodi hivyo kazi ilianza upya kabisa, lakini tulifanikiwa kwa asilimia mia-Alhamdulillah

Katika kipindi cha mwisho wa historia ya MTA ilipokuwa Morogoro walitumwa kutoka Markaz Maulana Faiz Nasir Ahmad (Head of Programing MTA Africa) na Mr Luqman

Endelea Uk wa 5..

Amri Abedi Studios

Kutoka uk. 4

Ahmad (Admin MTA Africa), wao walikuja kutoa mafunzo juu ya kurekodi makala mbali mbali na baadhi ya nidhamu za uendeshaji na utendaji wa kiofisi na pia kukamilisha taratibu za ujenzi wa Studio Jijini Dar-es-Salaam.

Baada ya matarajio na kusubiri kwa mda mrefu kuhamia Dar es salaam nuru ilianza kuonekana pale Bwana Hamad Malik (Engineer) alipokuja kutoka Ujerumani na kuona ujenzi unavyoendelea na kutoa maelekezo kisha kurejea, nasi huku tukaanza kutanguliza familia Dar-es-Salaam huku kazi za Studio zikiendelea Mjini Morogoro. Hatimaye tuliona mambo yanaanza kujiweka sawa yenyewe kwani ni maazimio yalisema mwezi wa saba tutakuwa tumeshahamia Dar-es-Salaam ila mambo yalianza kukaa sawa mwanzoni wa mwezi wa kumi. Ndipo vifaa kadhaa vilichukuliwa na kuletwa Dar-es-salaam na kazi za uhariri zikaanza kuendelea na mambo mengine madogo madogo, ndipo Bwana Hamad Maliki ambaye ni mhandisi aliyefanya kazi Ghana, Gambia na Burkina Faso katika kuandaa studio za MTA katika nchi hizo alirudi tena. Kazi ya kwanza ilikuwa ni kwenda kuondoa kila kitu huko Morogoro na kuvihamishia Dar es salam, tukio hili la kihistoria liliibua hisia za walioshiriki katika mchakato huu, kwa sababa zilitumika siku tatu tu Morogoro usiku na mchana, Mimi nilichoona ni kwamba tulienda tukafikia kufanya kazi, na ilikuwa hivi kwamba kazi ya kesho ilikuwa ngumu kuliko ya jana na baada ya kumaliza tu na kupandisha mzigo katika gari inayoleta Dar-es-salaam basi na sisi tulipanda Basi kwa pamoja na kuja kuwahi kushusha Dar-es-Salaam. “Hisia yangu imeniambia kuwa bila ya Huzoor (aba) hakuna chochote kinachowezakana, kupitia hili nimejifunza kuwa Allah anapitisha fadhila na baraka kwenye kivuli chake” alisema kijana mmoja aliyekuwa amehusika katika mchakato huu. Yapo mengi nimeyasikia na kuyahifadhi, mmoja alipoulizwa alisema kuwa “Kwa kifupi huu mchakato ulikuwa wa baraka tele za Allah, maana hali ilikuwa ngumu sana, na kazi ilikuwa ngumu lakini kwa msaada wa Allah ilikuwa nyepesi. Mimi binafsi nilipoona shani ya Allah ni pale tulipotakiwa kuondoa vifaa na kuvileta hapa Dar es salaam. Maana licha ya uchache wetu na uhaba wa uzoefu lakini kwa fadhila za Allah tulifanikisha kwa kiwango kikubwa sana. Hii inaashiria kuwa mpango huu ulikuwa na fadhila kuu na baraka tele kutoka kwa Mungu”. Ni hisia zinazouvuta moyo na za kweli kabisa kwani kupitia tukio hili ukilistadi kwa undani wake tumepata kujifunza mengi mno, “Katika tukio la kuhamisha studio kutoka Morogoro kuja Dar es salaam kwangu lilikuwa tukio la kipekee na linanikumbusha kuwa kila jambo lina wakati wake maana kuna muda ambao nilikuwa naufikiria na muda ambao tulifanikiwa kuhamisha ni vitu viwili tofauti. Na nimepata funzo kuwa subira ndio kitu kikubwa sana kawa mwaminio na kuwa jambo unaweza kuliona limekaa muda mrefu lakini ukilipata inakuwa ni kama umeliomba jana na leo Mungu kajibu maombi yako”. Hizi ni hisia za kweli za ndani katika mchakato huu na Alhamdulillah watu walifanya kazi kwa ushirikiano, vicheko na upendo mpaka studio mpya ya kisasa ikasimama katika maono yake halisi.

Na kwa ruhusu ya Hadhrat Amiir ul Muuminiin Khalifat ul Masih V (aba) Maulana Faiz Nasir Sahib alitumwa tena kwa ajili ya kuweka vifaa vipya vya ofisini na kufanya ufunguzi rasmi wa studio, na katika kipindi kuelekea ufunguzi siku moja kwa ajili ya mafunzo iliandaliwa na watu walishiriki ambao wanajitolea na walio tayari kujitolea katika studio hizi. Basi tarehe tajwa hapo mwanzo Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania pamoja na Wawakilishi kutoka Makao makuu walikata utepe na kufungua Studio mpya, baada ya hapo walizuru studio na kujionea vifaa vya kisasa na muonekano mpya wa studio. Hafla ilifunguliwa na usomaji wa Qurani tukufu uliofanywa Hafzi Zafurullah Ame na shairi lilosomwa na Mwalimu Mohammad Habibu. Katika hotuba yake Maulana Faiz Nasir alisema katika hotuba yake kuwa “Studio hii ambayo imezinduliwa leo inatarajiwa kutumika kama kituo cha MTA katika Afrika Mashariki na itatumikia nyenzo ya kutimiza bishara ya Masihi aliyeahidiwa (as) mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya isemayo “**Mimi Nitafikisha ujumbe wako mpaka pembe zoke za Dunia**”

Katika Hotuba yake Amiri na Mbashiri Mkuu alisema kuwa “Leo ni siku muhimu katika historia ya Jumuiya ya waislamu Ahmadiyya Tanzania kwa sababa studio yetu ya MTA inazinduliwa leo hapa Dar-es-Salaam tangu miaka miwili mitatu iliyopita tulikuwa tunaisubiria siku hii na leo ndio siku tumetimiza lengo hili” kisa Amiri na Mbashiri Mkuu aliwaomba watu kuwa tayari kwa ajili ya kujitolea wakati wao

Jamia yazidi kutoa Matunda

Na.
Mwandishi wetu



Picha ya pamoja ya Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib, kulia ni Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib, pamoja na wahitimu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro.

Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na kwa baraka za Khilaafate Ahmadiyya, vijana wetu wapatao tisa (9) wa Chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya kutoka katika Mataifa matatu ya Afrika Mashariki wamefaninikiwa kuhitimu masomo yao chuoni hapa Morogoro_mwaka 2022. Vijana hao ni kutoka katika Mataifa ya Tanzania, Kenya na Burundi, Al-hamdulillahi. Mahafali ya wahitimu hao yalifanyika siku ya jumatatu ya tarehe - 5/12/2022 na mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib Amir na mbashiri mkuu hapa Nchini. Hafla ilianza majira ya saa 1:00 jioni mara baada ya sala za magharibi na Isha zilizo saliwa kwa pamoja. Katika hafla hiyo, Qurani tukufu ilisomwa na Bw. Hussein Omari Mpenda na kufuatiwa na shairi la Kiurdu lililosomwa na bwana Athumani Libuyi. Kisha zilifuata hotuba fupi fupi katika lugha za kiarabu, kiurdu na kiingereza, ambazo zilitolewa na mwanafunzi wa Darasa la awali (Mumahida). Wanafunzi hao ni wale walioshinda katika mashindano ya kielimu. Kisha ilifuata taarifa (report) ya mwaka 2022 katika lugha za kiurdu na Kiswahili. Baada ya ripoti ya mwaka, lilifuata zoezi la kugawa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani, mashindano ya kielimu, michango, tablighi, waqa-re-amal n.k. kazi hiyo ilifanywa na Mheshimiwa Amir sahib. Baada ya ugawaji wa zawadi, zilifuata nasaha fupi kwa wahitimu na kwa wote waliohudhuria, nasaha hizo zilitolewa na mheshimiwa Amir Sahib, Naye baada ya Tash-huud, na Tawudh na Suratil-fatiha, Amir Sahib alisoma aya za 71-72 kutoka Suratil-Ahzaab na aya ya 3 kutoka katika Surat As-Saff na kisha kuwataka wahitimu wazingatie taq-wa na kuishi na kutenda sawa na mafundisho ya Qurani Tukufu na Sunna za Mtume Mtukufu[saw] na daima vitendo vyao viwe sawa na kauli zao. Pia alipongeza jitihada zinazofanywa na mkuu wa Chuo na jopo la wakufunzi wake katika kuinua na kuboresha kiwango cha elimu kwa wanafunzi. Baada ya hotuba ya muheshimiwa Amir Sahib, lilifuata neno la shukrani kutoka kwa Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib Mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya, katika maelezo yake, Mkuu wa chuo alisema, anamshukuru sana muheshimiwa Amir Sahib kwa ujio wake na hakuna cha kumlipa waila neno stahiki linalofaa kumtolea shukrani kwa hisani yake kubwa juu ya chuo, Wanafunzi na watumishi kwa ujumla. Juu ya elimu alisema, jitihada zinaendelea kufanywa ili kuboresha zaidi na zaidi kiwango cha elimu na Inshaallah mwaka (2023) mabadiliko bora zaidi ya kiwango cha elimu yataonekana. Baada ya neno la shukrani kutoka kwa mkuu wa chuo, mheshimiwa Amir sahib aliongoza maombi ya kimya na kufunga kikao. Hafla hiyo ilihitimishwa kwa chakula cha pamoja. Taarifa za mahafali haya zilitangazwa na kurushwa na vituo mbalimbali kama vile Abood Radio na tv n.k.



Amir na Mbashiri Mkuu akimpatia Zawadi mmoja kati ya Wahitimu, Jamia Ahmadiyya.

Bustani ya Washairi

JERAHA

Jeraha ulilopata, si wa kwanza si wa mwisho.
Ni wengi yamewakuta, mazito kutoa jasho
Subira waliivuta, leo wavuna korosho
Mwisho wa dhiki faraja, hakuna lisilokuwa

Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba
Kiwalani - Dar es salaam.

HAKIONI MIUJIZA
Huruma kizazi hiki, Viziwi hatushauriki
Kwa wema hatuhamasiki, Kwa tamaa hatushikiki
Upuuzini tu ashiki, Herini hatusimiki

Baraka wala muujiza, Zibariki nyoyo zetu
Hatuoni la kushangaza, Hadharani afe mtu
Twasifu kwa kunyamaza, Wala hatuchangamki

Tena hatuna heshima, Hatujifunzi hekima
Hatupembui kusema, Mahala wala adhama
Wala si wa kuinama, Tukikosa twahamaki

Wajeshi vazi usoni, Rohoni puuzi fuba
Tuna lugha za vyuoni, Maana ni tupu jaba
Lafudhi nyingi a'ini, Jinga Haini zandiki

Mwanzo tujenge shauku, Kujibadilisha nyendo
Tujifunze kila siku, Mapya kuboresha mwendo
Dhana mbaya tupa huku, Jiendeleze na hiki

Shunda Mshundia Wana
Daluni - Tanga

ATHARI YA VITA

1. Vifo kuzagaa
Damu tapakaa
Anga kuchakaa
Athari ya vita.

2. Vilema kujaa
Wajane bakia
Yatima enea
Athari ya vita

3.Makazi bomoa
Kabwa kiu njaa
Maradhi ugua
Athari ya vita

4.Nchi ikimbia
Haki kupotea
Unyama shudia
Athari ya vita

5.Watoto jifia
Wake ingilia
Vikongwe potea
Athari ya vita

6.Uchumi bomoa
Ulinzi kusua
Vurugu kujaa
Athari ya vita

7.gharama kukua
Mauzo kupoa
Kukosa bidhaa
Athari za vita

8.Uhuru pungua
Kosa ijumaa
Mateka kukaa
Athari ya vita

9.Shuleni zuwia
Tenga familia
Akili kupaa
Athari ya vita

10.Tumwombe jalia
Yetu maasia
Apate samea
Tulinde na vita

MASIHI OMARY
STAMBULI
KISAGWA

UONGOZI KAZI NGUMU

Asalaam wasalatu, ndugu na wasalimia
Ninaanza na waitu, kuiweka yangu nia
Ya kuwa kumbusha watu, katuka jamia
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Mi nilipoteuliwa, niliona kawaida
Lakini kila hatua, nina piga kwa shida
Ndipo nilipogunduwa, Mi niombe msaada
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Namuuliza Radhia, wapi mi naelekea
Ananambia tulia, Allah atakusaidia
Wewe utafute njia, kwake ya kusujudia
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Namuangalia Zena, yeye alivyo tulia
Na tabasamu mwanana, akiwa anahutubia
Ua niweke bayana, kiwa peke ye alia
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Muangalie Salima, yeye asivyo tulia
Kila siku asimama, Malezi kuelezea
Lakini bado wa mama, yeye twampuuzia
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Anatuhimiza Shungi, Kwa aya kutusomea
lakini sisi kwa wigi, pembeni twa jiendea
Twa mkimbilia mangi, Sikafu kutuuzia
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Hija kapewa jukumu, Mahubiri shikilia
Yeye atafuta hamu, ya chakula kujilia
Maana yaliyomo humu, Moyo ulisha yajua
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Kwenda kuhubiri dini, si jambo la kawaida
Maana humu duniani, kuna kila tafsida
Watakuliza nini, achotaka huyu dada
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Enyi mlo viongozi, Kamba hii shikilia
Muabuduni laazizi, yeye tawasaidia
Mola wetu laazizi , akiombwa yeye hutoa
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Mwisho nakalibilia, viongozi nawambia
Shida mtajipatia, wajibu kuvumilia
Ushindi utajipatia, kwa Allah kutegemea
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Huu ndi mwisho wangu, wa hili shairi langu
Namuomba Mola wangu, tuondolee ukungu
yasije toke mafungu, saidia Mola wangu
Uongozi kazi ngumu, nasema mwana wa Idd.

Zuhura Idd
Kitonga -Dar Es Salaam
Mtunzi Mtoto

Nasaha Tatu

Na.
Maulana Sheikh Shaban A. Shunda

Uwepo wa watu wa Mungu katika dunia hii ndio chanzo cha baraka zote, na ni kana kwamba dunia hii imeumbiwa wao nasi wengine tunafaidika tu kutokana na uwepo wao. Popote waendapo na wakanyagapo huwa wanaacha baraka za milele katika sehemu hizo. Mnamo mwaka 1988 ardhi ya Tanzania ilibarikiwa kutembelewa na Khalifa wa Mwenyezi Mungu kwa mara ya kwanza, mstari huu utakuja kuonyesha shani yake katika histori pindi uislamu utakaposhika hatamu ya kuiongoza dunia, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad rh Khalifa wa nne wa Masihi aliyeahidiwa aliizuru nchi hii, Rafiki yangu Maulana Wahab Adam wa Ghana Mwenyezi Mungu amrehemu alisema "Khalifa anapotembelea nchi yoyote basi hutoa dira ya maendeleo ya jumuiya kwa miaka hamsini ijayo". Bila shaka Tanzania pia ilipewa dira yake ila Mimi nataka kuweka mbele yetu nasaha tatu alizotupa Hadhrat Khalifat ul Masih wan ne rh ambazo aliziita mwenyewe kuwa ni nasaha kwetu, katika hutuba yake ya ijumaa ya mnamo 9 september 1988 alisema:

"Kwa ajili ya jamaat ya Tanzania na Jamaat zote nyingine na pia ni kwa ajili ya watu wote nina nasaha tatu ambazo nina matumaini kwamba mtazisikiliza kwa makini na mtashika ahadi ya kuzifuata na kuzikubali na kumuomba Mwenyezi Mungu kwamba awape nguvu ya kusimamia ahadi zenu.

Nasaha ya kwanza ni hii kwamba simamisheni sala, kuhusu mambo yanayohusiana na sala kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, kwa maono yangu ni kwamba kiwango cha usaliji wa hapa unaridhisha, ukilinganisha na mataifa mengine hapa kuna uzingatiaji mzuri wa sala, lakini ndani ya Qurani tukufu Mwenyezi Mungu hakutoa agizo kuhusu kusali bali alitoa muongozo juu ya kusimamisha sala, na kuhusu kusimamisha sala kuna mambo mengi yakuzingatia, sala ile ambayo itasaliwa bila uelewa hatuwezi kuuita kusimamisha sala kwasababu Qiyaam (kusimamisha) ni jina la kitu imara kusimamisha ni kitu kilichoambatana na kitu imara ambacho kina nguvu ya kusimama peke yake kwa miguu yake miwili. Hivyo basi ni lazima kuzitenda uzuri faradhi za sala na kuifanya uzuri misingi yake ni muhimu pia, kwa mnasaba huu Mimi natambua kwamba kwa ajili ya Jamaat zote inabidi tutengeneze utaratibu kwamba wasimsubiri mwalimu tu, bali yeyote Yule ambaye anaijua tafsiri ya sala na ni mcha Mungu na pia ana elimu kwa uchache, basi anatakiwa kuanzisha madrasa katika sehemu yake na kwa kutoa kipaumbele hasa kwa vijana wadogo kwamba wahifadhishwe tafsiri za sala kisawa sawa na ni lazima kuwashirikisha wakina Mama wa jumuiya katika programu hii, kama wakina Mama wenu na watoto wenu wa kike wataelewa vizuri tafsiri za sala na pamoja na hayo wataelewa mas'ala za sala kwa sababu kwa kusimamisha sala mas'ala za sala zinahusika moja kwa moja, ni namna gani udhu huvunjika, ni wakati gani ni lazima kuoga, ni vitu gani vinatakiwa kufanywa mwanzo na ni vitu gani vinatakiwa kufanywa baadaye, dua ni zipi, kuhusu sehemu ya kusalia, ni namna zipi za kusali sala kwa jamaa na mambo yake, haya ndio mambo yote ambayo yakikusanyika kwa pamoja

Endelea Uk wa 7..

Nasaha Tatu

Kutoka uk. 6

ndio husimamisha sala. Kwa hivyo basi ninapowaambieni msimamishe sala basi katika fikra zangu ipo programu yote hii kwa mapana yake. Kutokana na jambo hili pale ambapo yupo mwalimu basi kwa kipaumbele kabisa Mwalimu anatakiwa alishughulikie na pale ambapo hamna Mwalimu basi kama nilivyosema mtu yeyote mwenye elimu na Mcha Mungu anatakiwa aendeleze darsa hili na wakina Mama wasiachwe nyuma, na hili ndio jambo muhimu kabisa kama nilivyokuwa ninasema kwamba kama wakina Mama wenu na watoto wenu wa kike wawe wenye kusimamisha sala basi kwa fadhili za Mwenyezi Mungu mbeleni kwa miaka mingi baadaye vizazi vyenu vitakuwa salama, kwa sababu wanawake ndio wanaotia azma hii katika mioyo ya watu tokea utotoni majumbani.

Nasaha ya pili ni hii kwamba inatakiwa muendeleze mbele zaidi kazi ya mahubiri na kila muahmadiyya awe mwanaume au mwanamke, mkubwa au mdogo anatakiwa ajitahidi kwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwamba katika mwaka anatakiwa kufanikiwa kupata Muahmadiyya mwingine mmoja, katika mnasaba huu wale watu ambao hawana elimu wanaogopa na wanafikiria kwamba tutakapoongea na watu wengine tutawaeleza kitu gani, lakini kwanza kwa ajili ya kufanya mahubiri haihitaji kuwa na elimu kubwa, ukweli ni kwamba kama wewe una mapenzi na Mwenyezi Mungu na unafanya maombi kwa ajili yake na kuanza kuwaita watu katika kufanya wema basi katika maneno yako kupatikana Baraka maalum, katika maneno yako kutakuwa na uzito, na yatapewa nguvu, hivyo basi wale wanaofanya kazi ya kuita kwa Mwenyezi Mungu na wale wanaoita kwa Mwenyezi Mungu, wale ambao wana mapenzi pia ya Mwenyezi Mungu na moiyo yao mapenzi ya Allah yamekaa na pia wanafanya maombi, katika njia yake mtu huyo upungufu wa elimu hauwezi kujitokeza kamwe, hivyo basi inatakiwa mumtegemee Mwenyezi Mungu na kwa kufanya wema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa maneno nyoofu na kwa huruma anzeni kuwaita watu katika Uahmadiyya. Kuhusu mnasaba wa upungufu wa elimu, upungufu huo katika nyakati hizi unaweza kuondolewa kupitia **vijitabu** baadhi ya vijitabu ambavyo zimesheheni masomo ya kimahubiri vimetengenezwa kule Kenya ambavyo vinahadhi ya elimu nzuri, nanyi pia kulingana na hali zenu mnaweza mkajiandalia, kwa fadhili za Mwenyezi Mungu mna wabashiri wengi kutoka Markaz ambao wana elemu nzuri na malezi mazuri wanaofanya kazi hapa, na wengine kwa fadhila za Mwenyezi Mungu ni wazawa wa Tanzania ambao wanajua kiurdu na pia Kiswahili ambacho ni lugha yao na pia wana utambuzi juu ya lugha ya kiarabu, hivyo basi wao wanao huu uwezo kwamba kama wakiamua wanaweza anza kuandaa vijitabu vidogo vidogo vya kimahubiri ambavyo ni rahisi pia vyenye kueleweka kirahisi kwa watu wenye uelewa wa kawaida na badala ya kutoa hoja nzito nzito wanaweza kuchagua hoja mbili tatu ambazo ni rahisi kabisa na wanaweza kuzichambua kwa mapana kabisa, kama vijitabu vya namna hio vikisambazwa nchi nzima basi kwa fadhila za Mwenyezi Mungu vinazewaza kuleta faida kubwa sana.

Nasaha ya tatu ni hii kwamba inatakiwa muanzishe mawazo ya kuachana na imani potofu, pindi Jamaat au dhehebu au Jamaat yoyote ya Mwenyezi Mungu inapopiga hatua za maendeleo basi mbele yake huwa kuna hatari kadhaa, wakati mwingine imani potofu za kale kwa namna ile ile zinaishi na kuambatana na watu na namna hii huingia katika Jumaiya kama vile katika Jamii yenye afya aingiavyo mdudu anaye sambaza maradhi na namna hii imani potofu za nje huanza kuingia katika jumuiya za kiungu, jambo la pili ni hii kwamba baadhi ya jumuiya za kiungu mwanzoni imani potofu ziliingia ambazo kwa ajili ya dini ni mambo yanayoiangamiza, katika hafla ya maswali na majibu jana nimepata kutambua kuwa jamaat haikuwekea mkazo vilivyo katika jambo hili, hivyo basi naukumbusha uongozi kwamba inatakiwa wafanye utafiti katika nchi nzima kwamba imani gani potofu ambazo kinyume na mafundisho ya kiislamu zilizoenea ambazo inabidi zifanyiwe jihadi kuondolewa, na uongozi wa jumuiya inabidi uliangalie tena jambo hili kwa jicho la pili, basi nami kwenu ninyi ninaombi hasa ambao ni wanajumuiya wake kwa waume nawaomba mjiweke mbali na imani potofu na inatakiwa muwanasihi watu kuhusu kuacha maovu sio kwa ukali bali kwa upendo na mapenzi na kwa huruma na mliweke akilini jambo hili kwamba sisi tutaendelea kuamrisha yaliyo mema na tutazuia mambo mabaya.”

Na Shabani A Shunda
Mubaligh-e-Silsilah

Mbweha na zabibu

Mtandaoni

Kulikuwa na mbweha mwenye njaa na kiu msituni. Kitu maskini alikuwa kutafuta mawindo kwa masaa, bila kuwa na bahati yoyote.





Baada ya kutumia siku nzima kutangatanga msituni, aliweza kuona nguzo ya zabibu tamu, ambayo ilining’inia kutoka kwa mzabibu mrefu.

Mbweha, akiwa amekata tamaa, alitaka kuwafikia. Aliruka na kuruka, lakini hakuweza kufika kwao. Baada ya majaribio mengi, mbweha alichoka.



Bah, sijali tena. Jumla, kwa nini nataka kula zabibu hizo? Wana hakika kuwa kijani na mwamba mgumu! Acha mtu mwingine ale ... ‘

Na baada ya kusadikika kwake, **aliondoka akijiamini anastahili sana kutoa tunda lililokuwa likingojewa kwa muda mrefu**.

Maadili:

ikiwa jambo fulani haliwezi kufikiwa au linaonekana kuwa haliwezekani, usilaumu wengine au mazingira. Kila moja ina uwezo wake na, pia, mapungufu.

Unganisha Nukta



Biskuti za Tangawizi / Ginger Biskuits.

MAHITAJI.

Unga.
Cocoa ya unga.
Yai
Siagi.
Sukari.
Tangawizi mbichi.
Karafuu ya unga.
Baking soda.
Mdalasini ya unga.
Mollases.
Chumvi.

JINSI YA KUPIKA.

-Katika bakuli chunga unga, baking soda, chumvi na cocoa. Weka kando.
-washa oven lipate moto. Chukua bakuli jingine weka siagi na sukari.. changanya na mwiko hadi iwe imechanganyika vizuri.
-Mimina Mollases na Yai katika mchanganyiko wa Sukari na Siagi.. Weka unga kidogo kidogo mpaka utakapoweka unga wote.
-Mimina mdalasini,tangawizi na kaarafuu. Weka mchanganyiko wako kwenye friji kwa masaa mawili.
- Ukitoa tengeneza viduara vidogo vidogo,chovya kila kiduara katika sukari kisha weka kwenye trei la kuoka.
-Rudisha viduara kwenye friji kama nusu saa kisha weka kwenye oven kwa 350°F kwa dakika 15.
- Toa biskuti zako kwenye oven tayari kwa mlo.!



Malezi ya Watoto

Imetafsiriwa na
Sheikh Shahab Ahmad, Morogoro



بسم الله الرحمن الرحيم

Jiepushe na Ushirikina Fiche

Hadhrat Maulvi Abdul Karim sahaba mmojawapo wa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasimulia kwamba:

"Hudhur (as) alichukia sana kuwachapa watoto; mimi nilishuhudia mara nyingi kwamba yeye hajawahi kulikasirikia jambo lolote isipokuwa jambo hili tu ikiwa anapata taarifa kwamba mtu alimpiga mtoto. Mzee mmoja hapa alimpiga mwanaye kama ilivyokuwa kawaida yake basi Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alighadhibika sana na alieleza uchungu wake kwa kumwita yeye na akasema kwamba kwa mujibu wangu mimi kuwachapa watoto hivi ni sehemu ya ushirikina; kwani mjeuri anayechapa anapenda kujijumuisha katika (sifa za) kutoa mwongozo na malezi. Akasema: Mtu mwenye jazba anapotoa adhabu kwa kosa lolote basi kwa kuongezeka katika hamaki hugeuka kama adui na huwa anapita kiasi katika kutoa adhabu kuliko kosa lenyewe.

… Akasema: Jinsi ambavyo jitihada hufanyika kutoa adhabu, laiti wangalishughulika na kufanya dua na wajipangie kabisa sehemu moja ili kuwaombea watoto kwa uchungu wa dhati. Kwa sababu dua za wazazi kwa ajili ya watoto hukubaliwa kwa namna mahsusi.

… Kisha Akasema: Kutoa mwongozo na malezi sahihi ni kazi ya Mwenyezi Mungu. Kufuatilia sana au kupita kiasi katika kusisitiza jambo yaani kuwakanya watoto na kuwakemea kwa kila jambo huonesha kwamba sisi ndio wamiliki wa kutoa mwongozo nasi tunaweza kumweka (mtoto) sawa kama tunavyopenda. Hii ndiyo aina mojawapo ya ushirikina fiche ambao kwao Jumuiya yangu hupaswa kuepukana nao. Alisema kinagaubaga na aliandika kabisa amri yake kwamba katika shule yetu mwalimu ambaye ana kawaida ya kuwachapa watoto na hakomi kufanya kitendo chake kibaya basi mnatakiwa kumfukuza kazi mara moja. Akasema: Mimi huwa ninafanya dua kwa ajili ya watoto na huwa ninawafanya wazingatie sheria na adabu za kawaida, basi ni hiyo tu hakuna cha kuongeza; vilevile huwa ninamtegemea kikamilifu Allah subhanahu wataala (kwani) namna ambavyo mtoto atakuwa na mzizi wa saada atakuwa vizuri kwa wakati wake."

(SIRAT HADHRAT MASIHI MAUDas kur. 37-38)

Allah atujalie kuzingatia na kuufanyia kazi mwongozo huu. Aamin.

Utambuzi wa Mwanajamaat Ahmadiyya

Haya ndiyo yale mambo na yale masharti niliyokuwa nikiyasema tangu mwanzo. Kila Mtu anayetokana na Jamaat yangu atalazimika ashikamane na wasia wote huo, na inapaswa kusiwe na shughuli yoyote chafu yenye mzaha na kejeli kwenye vikao vyenu, na tembeeni ardhini kwa moyo mwema, mwenendo uliotakasika na mawazo yaliyotakasika. Na kumbukeni kwamba sio Kila Shari kupaswa kukabiliana nayo, hivyo ni Lazima kwamba mara nyingi muwe na kawaida ya kusamehe na kuachilia, na fanyeni Subira na Upole na msimshambulie yeyote kwa njia isiyojuzu na myadhibiti Matamanio ya Nafsi. Na mkifanya majadiliano au mazungumzo ya Kidini basi mfanye kwa Maneno laini na njia ya kistaarabu. Na kama yeyote akiwafanyia ujinga basi toeni salamu na haraka muondoke kwenye kikao hicho. Mkisumbuliwa na kutukanwa na msemwe kwa lugha chafu, basi muwe macho kwamba msikabiliane na ujinga kwa ujinga, waila ninyi nanyi mtakuwa wa aina hiyo hiyo kama walivyo. Mwenyezi Mungu Anataka kukufanyeni muwe Jumuiya ya aina hii kwamba muwe Mfano wa Wema na Ukweli kwa Dunia nzima. Hivyo, mumuondoe kwa haraka sana toka miongoni mwenu Mtu yule aliye Mfano wa Uovu, Shari, uchochezi wa fitina na tabia mbaya. Yule Mtu asiyeweza Kuishi ndani ya Jumuiya yetu kwa Unyenyekevu, Wema, Kujizuia, Upole, lugha ya Upole, tabia njema na mwenendo mwema, yeye haraka sana atengane nasi, kwa sababu Mungu wetu Hataki Mtu huyo abaki miongoni mwetu na kwa yakini yeye atakufa akiwa mwenye bahati mbaya kwa sababu yeye hakuichagua njia ya Wema. Hivyo tahadharini na muwe hasa wenye mioyo Mema, wanyenyekevu na wakweli. Ninyi mtatambuliwa kwa Sala tano na khulka njema, na yule ambaye ndani mwake mna mbegu ya Uovu, hataweza kuendelea kushikamana na nasaha hii. (Majmu›ah Ishtihaaraat, J. 3, uk. 46 - 48 Ishtihaar, tarehe 29 Mei 1898)

MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA PICHA



Picha ya pamoja inayomuonesha Amir na Mbashiri Mkuu, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, akiwa na wahitimu wapatao 9 na watumishi wa chuo hicho cha Jamia Ahmadiyya Tanzania, siku ya Jumatatu ya Tarehe 05/12/2022



*Picha ya pamoja inayomuonesha Marehemu **Muhammad Saeed Lone wa kwanza kulia katika viti**, wa pili Muhammad Iqbar Dar, tatu Sheikh Waseem Ahmad Chima, nne Sheikh Faiz Sahib, tano Mahmood Alshad Sahib, sita Sheikh Yusuph Kambaulaya Sahib. Pamoja na Sheikh Bakr Abeid Kaluta Sahib wa kwanza kulia, pili Sheikh Abdul-Nasir Sahib, tatu Sheikh Murtaza Sahib, nne Sheikh Mahmood Bhutti, tano_____, sita Sheikh Mubarak Sahib, saba Sheikh Tabassam Sahib na Sheikh Karimu-ddin Shamsi Sahib.*

Buriani Muhammad Saeed Lone

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Dar



Muhammad Saeed Lone

Katika hotuba yake ya Ijumaa katika Masjid Salaam – Dar es Salaam, Khalifatul Masih wa (iv) Hazrat Mirza Tahir Ahmad[ra] ikiwa ni mara ya kwanza Khalifatul Masih kutembelea Tanzania, alisema *"kuna mvuto wa aina yake katika ardhi ya nchi hii kwani. Wote walio wa kuishi hapa wanaikumbuka na kuipenda sana, nchi hii"*. Miongoni mwa hao ambao daima alijihisabu ni mzalendo wan chi na kuipenda kwa mapenzi makubwa ni Muhammad Saeed Lone mwana wa Fadhil Karim Lone ambaye ametutoka Tarehe 06/01/2023 na kutuacha na majonzi makubwa, sisi ni wa Mwenyezi Mung una kwake tutarejea.

Muhammad Saeed Lone alizaliwa mnamo Tarehe 09 mwezi Machi 1932. Alipata elimu yake mjini Dar es Salaam na Mwaka 1951 akajiunga na shirika la Posta la Afrika Mashariki, ambako alifanya kazi kwa miaka Ishirini. Mwaka 1954 alioa na katika ndoa hiyo alijaliwa kupata Watoto wafuatao, Jahida alizaliwa 1955, Razia 1957, Masood aliyezaliwa 1959 Dodoma, Razia Nazr alizaliwa 1962 Iringa.

Mwaka 1958 ulikuwa wa msukosuko kwa Muhammad Saeed Lone, baada ya binti yake Razia aliyezaliwa 1957 alipofariki. Wakati huo Wanajamati mjini Dodoma walikuwa wakuhesabiwa kwenye kiganja, Sunni walikataa kata kata binti huyo kuzikwa katika makaburi yao. Wanajamati waliwaendea Waismailia ambao walikubali kwa moyo mkunjufu binti kuzikwa katika makaburi yao.

Disemba 1972, Muhammad Saeed Lone alihamia Uingereza na kujiunga na Kampuni ya Ford Mota Company na 1972 akastaafu. Toka alipostaafu alijitolea muda wake wote kuitumikia Jumuiya ya Ahmadiyya. 1995 alikuwa Raisi wa Jamati ya Naltham Forest East London. Mwaka 1988 alikuja na Huzur, wakati Huzur alipotembelea Tanzania kwa mara ya kwanza. Kutoka wakati huo Muhammad Saeed Lone alifanya ziara za mara kwa mara kuitembelea Tanzania. Katika safari hizo alishirikiana na ndugu yake Mubaraka Lone kujenga Msikiti na nyumba ya Mbashiri kule Dodoma. Msikiti huu katika makao makuu ya nchi ulifunguliwa na Khalifatul Masih wa (iv)[ra]. Msikiti wa Mkuyuni aliukarabati na Huzur akaupa jina Tahirah.

Muhammad Saeed Lone alipenda sana vijana wa Jamati wapate elimu. Nakumbuka nikiwa Katibu wa elimu aliweza kutoa misaada kwa wanafunzi uliowasaidia kununua vitabu na vifaa vingine muhimu katika masomo yao.

Mahubiri ndio kilikuwa kikombe chake cha Kahawa, alipenda Mahubiri. Alikuwa akitoka na Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiswahili na kuiuza mitaani. Kwa gharama yake alichapisha kijitabu ***Kifo juu ya Msalaba Hoja kumi kutoka Biblia Takatíbu, utungo wa Maulana Abul Ataa.*** Kijitabu hiki alikigawa bure, Muhammad Saeed Lone ameandika Kitabu ***Life of Muhammad***, ambacho kwa lugha nyepesi naya kuvutia kinaeleza Maisha ya Mbora wa viumbe wote Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Ni alama kubwa ya Mapenzi na hatuna ufaulu mkubwa kuliko kumpenda Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Melezo Zaidi yatatolewa Inshallah katika toleo lijalo.

Somo Toka Maisha ya Dr. Iddi Ibrahim Mwanga



Dr. Iddi Ibrahim Mwanga

Ni dhahiri ya kwamba hakuna miongoni mwetu aliyeamua kuja huku kama hatukuamua, hatuwezi katu kufahamu shabaha ya kuja huku na wala hatuwezi kufahamu siku ya kuondoka. Bila shaka yupo aliyetuleta, aliyetuumba ndiye anafahamu shabaha ya kutuumba. Kitakuwa kichekesho. Mshairi anatuzamisha katika swali la msingi ambalo wanafalsafa wamekuwa wakijaribu kulitafutia jibu lake bila mafanikio. ***Ati yuko fundi na akilize, pasipo kusudi atengeneze, vyombo vya ajabu avifanyize, visiwe na kazi viifanyayo? Swali hilo analijibu, kamuumba mtu aendeleze, sifa zake njema aziigize, yaliyo maovu ayakataze, itue amani itulizayo***. Madhumuni ya kuumbwa kwetu ni kumuabudu Allah[sw] na kutoa haki kwa viumbe wake. Ni shabaha hii aliyoizingatia Dr Mwanga katika maisha na ikampatia utulivu na amani.

Mtizamo na falsafa ya kutoa kwa upande wa Dr. Mwanga ilikuwa pana na ndefu. Aliamini kuwa tunajidanganya kuwa tunatoa, sisi ni wapokeaji, utatoa nini? Tunalipa deni, nalo tunapunguza tu hatulipi lote. Alisema tazama jua linavyotoa tena kila siku mwanga wake.

Na jua hilo linawaka na kutoa mwanga pasi kuchagua wanakoishi wenye uwezo na akina kacheku, akina yakhe weka mchuzi pangu pakavu!

Hakuna masimango, hakuna masimulizi. Miti inatoa matunda na sisi tunachuma, bahari inatoa samaki tunafaidika, ng'ombe anatupa maziwa tunakunywa, nyama tunakula, ngozi tunatengeneza viatu na mbolea tunatumia mashambani. Hakuna maisha bila kutoa. Usitoe ili uonekane, toa ili upate furaha ya moyoni. Hakuna maisha bila kutoa. Itatoka wapi hofu ya kiu ikiwa kisima chako cha yakini kuwa mtoaji hasa ni Allah kimejaa? Wenye kidogo nao watoe, ni alama ya imani yao kuwa Mtoaji atawapa kingine. Wanatoa kwa furaha malipo yao ni furaha na wanaotoa shingo upande kwa uchungu malipo yao ni uchungu. Ni vizuri kutoa unapoombwa lakini ni vizuri zaidi kutoa kwa kuelewa maumivu ya yule unayempa. Toa mwenyewe na usipotoa hivyo vilivyo vyako vitatolewa na wengine. Kwa nini usitoe ukapata thawabu kwa kutoa wewe mwenyewe? Ni mawazo mazito aliyoyatoa Dr Iddi Ibrahim Mwanga. Maendeleo na mabadiliko yote tunayoyaona yametokana na utamaduni wa kutoa.

Ukipita kwenye mti wenye matunda kochokocho hutakosa kujionea mti huo ulivyoinama kwa wingi wa matunda. Dr Mwanga alikuwa ni mti ulioinama. Hakuwa na majivuno wala kiburi. Elimu yake haikumfanya atembee katika ardhi kwa maringo, mikogo na daima alikiri kuwa hajui na hivyo akaongeza bidii ya kujua. Unawezaje kufikiri kuwa wewe unajua wakati. Allah Ameeleza, kwa kila anayejua yupo anayejua zaidi. Maisha ya upole, unyoofu, yasiyo na mbwembwe na kiburi huvuta wa mbali na karibu ili wakafuate wewe. Mwenendo huu uliwavuta wengi wawe karibu na Dr Iddi Ibrahim Mwanga.

Binadamu ni mwepesi wa kushauri wengine, kuwaonyesha njia wengine, kuwakemea, kuwalaumu na kwa kufanya hivyo kuisahau nafsi yake. Matokeo yake kila unayoyasema, unayoelekeza, unayoshauri yanapuuzwa kwani binadamu huathiriwa zaidi kwa vitendo kuliko maneno usemayo. Ni taswira nzima ya maisha ya Dr Mwanga yaliyowavuta wafanyakazi wenzake, wanajamati na wanae kumheshimu na kusikiliza aliyokuwa anasema. Heshima kubwa ya binadamu imejengeka katika vitendo na sio maneno, kwani ni ukweli usiopingika kuwa ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo.

Kazi ndio hassa kielelezo cha utu wa binadamu. Kazi si laana bali neema. Lakini ifanywe kwa mapenzi na shauku kubwa. Kufanya kazi ili kutimiza mradi haitusaidii sana. Tupende kazi tukipamba kazi kwa mapenzi. Upatikane utam katika kazi tunazozifanya. Nakumbuka akisisitiza juu ya umuhimu wa mapenzi ya kazi, Dr Iddi Mwanga aliwahi kumnukuu mwandishi maarufu wa Lebanon, Khalil Gibran ***'kama huwezi kufanya kazi kwa mapenzi bali kwa kinyongo, ni heri kuacha kazi hiyo na ukae nje ya mlango wa hekalu ukiomba sadaka kutoka kwa wale wanaofanya kazi kwa furaha'***.

Islam inafundisha kuwa kila binadamu anaweza na kwa hakika inambidi kuanzisha mawasiliano baina yake na Muumba wake. Ni mawasiliano yanayojenga mapenzi na yakini. Kurasa za maisha ya Dr Iddi Ibrahim zinatufundisha kuwa milango iko wazi kwa yule anayemtafuta Muumbaji kwa dhati na shauku. Ukishampata Mola wako unakuwa ni mtu anayetawaliwa na fikra njema na Shaaban Robert anamsadifu vilivyo mtu wa namna hiyo;

Mtu wa fikra njema, kwa watu huacha jina
Na watu wajao nyuma, wakapenda kuliona
Katika Dunia nzima, ikawa kubwa hazina.

(Kutoka kwenye Mswada wa Kitabu ***Maisha ya Iddi Ibrahim Mwanga (1947-2020)*** Daktari wa Mwili na Roho) - ***Mahmood Hamsin Mubiru.***

Kutoa Katika Njia ya Mwenyezi Mungu: Waqfe Jadid 2023

Kutoka uk. 12

Mwenyezi Mungu], ambamo Mwenyezi Mungu alimwambia Mtukufu Mtume (saw) kwamba baada ya watu kutoa mali kwa Mungu, wabakie na utulivu, kwani hakuna hofu ya kuchomwa moto au kuibiwa, bali ni salama. Mali yoyote aliyopewa Mwenyezi Mungu itarudishwa siku ambayo mtu huyo anaihitaji zaidi. Kwa hivyo, sio tu kwamba dhabihu za kifedha zinamsaidia mtu hapa duniani, bali na akhera pia. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'ani Tukufu:

Na mali yoyote mtakayotoa, mtarudishiwa sawasawa, wala hamtadhulumiwa. (Qur'ani Tukufu, 2:273).

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Mwenyezi Mungu anapotoa ahadi, Yeye huitimiza. Anaonyesha utimilifu wa ahadi yake hapa duniani, ili mtu aridhike akijua kuwa nayo itatimia Akhera. Si kama biashara za kilimwengu ambapo mtu anaweza kuwekeza pesa zake, na kuzipoteza, baada ya muda mfupi tu wa uwekezaji. Mashirika huchukua sehemu kubwa ya mali, na kuwaacha watu kupoteza sehemu kubwa ya uwekezaji wao, kama ilivyotokea hivi karibuni kwa watu kupoteza mabilioni ya bitcoin na cryptocurrencies. Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa kwa vyovyote vile, anachukulia cryptocurrencies (sarafu ya siri) kuwa ni aina ya kamari.

Mifano ya Ajabu ya Mwenyezi Mungu Kuwalipa wanaojitolea katika Njia Yake

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba atataja mifano ya watu wanaotoa dhabihu za kifedha ambazo sio tu zinawawezesha kupata thawabu, bali imani yao pia inaongezeka.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kuna mfano kutoka Liberia ambapo mwalimu mmoja alikwenda katika kijiji kipya kilichojiunga hivi karibuni kwa ajili ya kukusanya mchango wa Waqf-e-Jadid. Kulikuwa na kijana ambaye alienda nyumbani kuleta pesa, hata hivyo mama yake alisema kuwa hawana chochote. Kisha, kijana huyo akaja mbio akisema kwamba alikuwa na dola 250 za Kiliberia ambazo baba yake alikuwa amempa kwa ajili ya karo yake ya shule, hata hivyo hakutaka familia yake kubaki bila baraka hii ya kujitolea. Muda mfupi baadaye, kijana huyo alisema kwamba jamaa yake alimpa dola 2500 za Kiliberia ili kulipia karo yake ya shule. Hivyo, mchango alioutoa uliongezwa mara kumi.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa nchini Tanzania kuna mwanamke mmoja alikuwa ameenda sokoni. Akiwa njiani, alikutana na mwalimu wa eneo hilo ambaye alimwambia kuhusu Waqf-e-Jadid. Alikuwa na shilingi elfu mbili mkononi na hivyo akatoa elfu moja kwa mwalimu wa eneo hilo na kusema kwamba angetumia iliyobaki kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani. Muda mchache tu baadae, bibi mwingine alimwita, na akagundua kuwa huyo ni bibi ambaye alikuwa amemkopesha shilingi elfu tano muda mrefu uliopita na alikuwa amepoteza matumaini ya kuzipata tena. Hata hivyo, muda huo huo bibi huyo alifika kwake na kumrudishia kiasi cha shilingi elfu tano. Baada ya kutokea hili, mara moja alirudi kwa mwalimu wa pale na kumwambia kwamba hii ilikuwa tu kwa sababu ya baraka za kutoa dhabihu za kifedha, na akatoa shilingi elfu moja zaidi kwa ajili ya Waqf-e-Jadid.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Ahmadiyya mmoja kutoka Nigeria alikuwa akitafuta kazi kwa miaka mitatu lakini hakufanikiwa. Kwa sababu ya kutokuwa na kipato, hakuweza kutoa mchango wa kifedha, lakini aliamua kwamba anapaswa kutoa dhabihu ya kifedha kwa mara nyingine tena. Miezi mitatu tu baada ya kuanza kutoa dhabihu za kifedha, alipata nafasi ya kazi kutoka kampuni fulani.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba huko Togo, kuna mtu ambaye hakuwa na pesa nyingi na ulikuwa mwezi wa mwisho wa mwaka wa Waqf-e-Jadid. Alikuwa na mbuzi mdogo nyumbani na alikusudia kumuuza na kutumia pesa hizo kutoa mchango wake. Wakati huo huo, mwalimu wa huko alimwendea kuchukua fedha kwa ajili ya Waqf-e-Jadid. Ilikuwa pia wakati huo, ambapo mtu ambaye mtu huyu alikuwa amemkopesha pesa lakini akapoteza matumaini ya kurudishiwa, alikuja kwake na kumrudishia kiasi hicho. Kisha akatoa kiasi hicho chote kwa ajili ya Waqf-e-Jadid.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mtu huyu alikuwa amekusudia kutumia kutoka katika mali aliyoipenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na hii ndiyo njia ambayo Mwenyezi Mungu alimsaidia.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mwanamke mmoja kutoka Mauritius alisema kwamba alipokea kiasi kutoka kwa wazazi wake kama zawadi. Alikuwa ameiweka katika bahasha mbili zenye 500 kila moja kwa nia ya kuitoa kama dhabihu ya kifedha. Wakati huohuo yeye pia aliugua, na baadhi ya watu wa ukoo walikuja kumwona. Walimletea bahasha mbili zenye 5000 kila moja, na hivyo kuongeza kile alichokusudia mara kumi.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mtu mmoja nchini Indonesia alisema kwamba amepoteza kazi yake na mwaka wa Waqf-e-Jadid ulikuwa unaisha na hakuwa na uwezo wa kutosha wa kifedha kutimiza ahadi yake. Aliomba sana na alimwandikia Khalifa mtukufu (atba) kwa ajili ya maombi. Kwa namna fulani, aliweza kukusanya kiasi cha ahadi yake na kukitoa kwa ajili ya Waqf-e-Jadid. Siku chache tu baadaye, alipokea simu ya kupata nafasi ya kazi ambayo ilishangaza kuipata licha ya umri wake mkubwa. Walakini kwa sababu ya baraka hizi, aliweza kupata mapato ya uhakika.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Ahmadiyya mmoja kutoka Gambia alilazimika kushughulikia mambo yanayohusiana na kijiji chake, kwa vile baba yake asiyekuwa Ahmadiyya alikuwa chifu lakini alikuwa mgonjwa. Shirika moja la Kiislamu lisilo la kiserikali (NGO) lilikwenda kijijini kwake na kusema kwamba wanapenda kuchangia Dalasi 30,000 kwa kijiji hicho, hata hivyo hawatoweza kumpatia kwa sababu yeye ni Ahmadiyya. Kama angeacha Uahmadiyya wangeweza kumpa kiasi hicho. Aliwajibu akisema kuwa hahitaji pesa zao kwani Mungu ndiye Mpaji. Alisema hataiacha Jumuiya ya Ahmadiyya, kwa hakika aliwaambia kuwa anatoa Dalasi 15,000 kila mwaka kwa Jumuiya kama mchango wake wa kifedha. Walishangaa kusikia hivyo na kuuliza kwa nini aliweza kufanya hivyo licha ya kuwa maskini naye akawajibu kwa kusema kwamba laiti wangejua baraka anazopata kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi na wao wangejiunga na Jumuiya hii.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba hii ndiyo njia ambayo Mungu huwapa imani thabiti hata wale wanaoishi kwenye maeneo ya mbali vijijini.

Hii ni mifano michache tu ya matukio mbalimbali yaliyotolewa na Khalifa mtukufu (atba).

Ripoti ya mwaka 2022 na Tangazo la Mwaka wa 66 wa Waqf-e-Jadid

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba atawasilisha baadhi ya takwimu za mwaka uliopita wa Waqf-e-Jadid. Kwa rehema za Mwenyezi Mungu, mwaka wa 65 wa Waqf-e-Jadid ulimalizika tarehe 31 Disemba. Jumuiya ilichangia zaidi ya pauni milioni 12.2 kama dhabihu, ikiwa ni ongezeko la pauni 928,000 kutoka mwaka jana, licha ya hali ngumu ya kifedha duniani.

Orodha ya nchi katika suala la ukusanyaji ni kama ifuatavyo:

1. Uingereza
2. Canada
3. Ujerumani
4. Marekani
5. India
6. Australia
7. Nchi ya Mashariki ya Kati
8. Indonesia
9. Nchi ya Mashariki ya Kati
10. Ubelgiji

Kwa upande wa asilimia ya wale waliochangia kiwango kikubwa kwa kila mtu mmoja mmoja (per capita), nafasi ni kama ifuatavyo:

1. Marekani
2. Uswisi
3. Uingereza
4. Australia
5. Kanada

Nchi zinazoongoza barani Afrika katika michango ya Waqfu Jadid ni kama ifuatavyo:

1. Ghana
2. Mauritius
3. Nigeria
4. Burkina Faso
5. Tanzania
6. Liberia
7. Gambia
8. Uganda
9. Sierra Leone
10. Benin

Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa mwaka huu, kulikuwa na ongezeko la wale wanaotoa michango ya watu 61,000 na kufanya jumla ya ushiriki kuwa watu milioni 1.56.

Khalifa mtukufu (atba) aliwasilisha orodha za Jamaat mashuhuri kutoka nchi zinazoongoza kimchango.

Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu awabariki wale wote waliojitolea muhanga wa michango ya kifedha.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAJAB - SHABAN. 1444 AH | FEBRUARI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume[saw] akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Kutoa Katika Njia ya Mwenyezi Mungu: Waqfe Jadid 2023

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatihah, Khalifa mtukufu (atba), Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisoma aya ifuatayo ya Qur'ani Tukufu:

'Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi hakika Allah Anakijua. (Qur'ani Tukufu, 3:93).

Kufikia Uchamungu kwa Njia ya Kujitolea Kifedha

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba alipokuwa akiifafanua aya hii, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba wema wa kweli ambao unaongoza kwenye wokovu hauwezi kupatikana mpaka mtu atumie kutoka kile anachokipenda kwa ajili ya ubinadamu. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba hivyo, huu ndio umuhimu mkubwa ambao Mwenyezi Mungu ameutoa kwa kujitolea dhabihu ya kifedha, kwa kiwango ambacho bila hiyo, hatimaye mtu hawezi kupata wokovu.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba dhabihu ya kweli ya kifedha sio kutumia kutoka kile ambacho mtu alikuwa tayari hakitumii, badala yake ni kutumia kutoka kwenye mali ambayo tunaipenda zaidi, na kufanya hivyo kwa upendo



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tanoatba akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 06 Januari, 2023. Akieleza Umuhimu wa Kutumia Kati ya kile Upendacho na Tangazo la Mwaka wa 66 wa Waqf-e-Jadid'

kwa wanadamu. Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kuwa kutumia na kutoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu ni dalili ya Uchamungu wa mtu. Hadhrat Abu Bakr[ra] alikuwa ni mfano mkuu wa hili, kwani hitaji lilipotokea, alijitolea vyote alivyokuwa navyo nyumbani kwake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba wakati wa zama za Masihi Aliyeahidiwa[as], lilipokuja suala la kujitolea mhanga kwa ajili ya kueneza Uislamu, mfano mkubwa kabisa uliowekwa ulikuwa wa Hadhrat Hakim Maulvi Nooruddin (ra). Wakati fulani alimwandikia Masihi Aliyeahidiwa (as) akisema kwamba kama mali yake yote ingetumika kwa ajili ya Uislamu na uenezaji wake basi angefikia lengo lake. Pia walikuwepo Masahaba wengine wengi wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ambao walitoa dhabihu za kifedha.

Kwa nini walifanya hivyo? Ili kuwa wasaidizi katika ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na kazi zake.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba katika taasisi ya Ukhalifa iliyofuata baada ya Masihi Aliyeahidiwa (as), wakati wa zama za kila Khalifa, kuna mifano isiyohesabika ya wale wanaotoa dhabihu za fedha za kuwa mfano.

Madhumuni ya Mpango wa Waqf-e-Jadid

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kwa kawaida, hotuba ya kwanza ya mwezi Januari inatumika kutangaza mwaka mpya wa Waqf-e-Jadid. Huu ni mpango ambao ulianzishwa na Khalifa wa Pili Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahamd (ra) mwaka 1957 kwa madhumuni ya awali ya kueneza Uislamu katika maeneo ya vijijini nchini Pakistan. Baadaye, katika wakati wa Khalifa wa Nne (rh), dhana hii ilipanuliwa kwa nchi zote. Aliagiza kuwa mali iliyokusanywa chini ya mpango huu kutoka nchi tajiri itumike kwa nchi zinazoendelea kama vile Afrika. Hii pia haimaanishi kwamba wale wanaoishi katika nchi zinazoendelea hawachangii, badala yake dhabihu zao ni za kupongezwa. Wale wote wanaojitolea muhanga wanaelewa yale ambayo yametajwa katika Hadith-e-Qudsi [maneno ya Mtukufu Mtume (saw) kama ilivyoteremshwa kwake na

Endelea uk.11



Serikali ya Uingereza & Jihad

- Jihad ni nini na kwa nini Uislamu ulilazimishwa kuamua kujitetea mapema historia?
- Kwa nini wana fikra potofu kuhusu jihad kukita mizizi katika akili za baadhi ya Waislamu makundi na sehemu gani wana Waislamu makasisi na makasisi wa Kikristo walicheza mchakato huu?
- Je, ni halali kwa Muislamu kufanya maasi dhidi ya serikali inayosimamia sheria na utaratibu na kuruhusu uhuru wa kidini?

Maswali haya, ambayo yamekuwa lengo la umakini wa ulimwengu nipote leo, ulijibiwa tena miaka mia moja iliyopita kwa mwongozo uliotolewa na Mungu na kuelewa kwa mtu aliyedai kuwa Masihi Aliyeahidiwa.

Nakala hii itapatikana kwa bei ya Sh. 2,800/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com